**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## BENKI KUU YA TANZANIA

**10 Januari 2025**

### TAARIFA KWA UMMA

### CANARA BANK TANZANIA LIMITED YAHAMISHA MALI NA MADENI YAKE KWENDA EXIM BANK TANZANIA LIMITED

Taarifa inatolewa kuwa Benki Kuu ya Tanzania, kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu namba 30(1)(b) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imetoa idhini kwa Canara Bank Tanzania Limited kuhamisha mali na madeni yake kwenda Exim Bank Tanzania Limited, na vilevile kuacha kufanya biashara ya kibenki kuanzia tarehe 20 Desemba 2024. Hivyo basi, kuanzia tarehe 21 Desemba 2024, wateja wa iliyokua Canara Bank Tanzania Limited watahudumiwa na Exim Bank Tanzania Limited.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya kibenki.

**EMMANUEL M. TUTUBA**

**GAVANA**